# MAPENDEKEZO YA TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR

# RIPOTI YA UTAFITI WA SHERIA YA MAADILI NAM 4 MWAKA 2015 ZANZIBAR

**INAWASILISHWA KWA MHESHIMIWA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA**

**MWAKA, 2022**

**JUNI, 2022**

# SURA YA SITA

## 6.0 MAPENDEKEZO NA HITIMISHO

Baada ya kufanya utafiti huu, kufanya tathmini, kuzingatia maoni ya wadau, kuangalia uzoefu wa nchi mbali mbali zilizoainishwa katika utafiti huu, Tume inapendekeza yafuatayo:

### 1.1MAPENDEKEZO YA KISHERIA

1. Kuimarisha mfumo mzima wa kisheria wa kusimamia maadili ya Viongozi wa Umma kwa kuutekeleza kwa mujibu wa Sheria (enfocement).

2. Muundo wa Tume ya Maadili uliopo hivi sasa unatoa changamoto nyingi za kiutendaji kwani hakuna mgawanyo wa majukumu na imeonekana kuwa majukumu yote kuanzia kupokea malalamiko, kuchunguza na kuyasikiliza pamoja na kuyatolea maamuzi, yote yanafanywa na Mwenyekiti wa Tume hiyo. Hivyo, Tume ya Kurekebisha Sheria inapendekeza
   a) Muundo uliopo hivi sasa urekebishwe na uwe muundo ambao utagawanya kazi na madaraka ndani ya Tume. Hivyo, kuanzishwe kitengo ambacho kitapokea malalamiko na kuyafanyia kazi kwa kuyachunguza kisha kuwasilisha mapendekezo yao kwa Tume ambayo itaongozwa na Mwenyekiti na Makamishna.
   b) Kitengo hicho kitakachoanzishwa ni vyema kikaongozwa na Kamishna maalumu ambaye anaweza kujulikana kama Kamishna wa Maadili. Aidha, baada ya kitengo hicho kufuatilia malalamiko, kitawasilisha taarifa yake kwa kitengo chengine ambacho kitajulikana kama Tume, ambayo itakaa na pande zote mbili na kutoa maamuzi na mapendekezo Serikalini. Kitengo hiki cha pili (Tume) ndio kitakuwa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma na kitaongozwa na Mwenyekiti pamoja na Makamishna wake.

c) Inapendekezwa katika Sheria hii kiongezwe kifungu ambacho kitanzisha Kitengo cha Maadili pamoja na kuwepo kwa Kamishna wa Maadili. Aidha, kifungu kidogo kioneshe uteuzi wake pamoja na kazi zake.

3. Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma ya hivi sasa haina kifungu ambacho kinamlinda mtoa taarifa dhidi ya Kiongozi aliyemlalamikia. Hivyo, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza kuwepo kwa kifungu ndani ya Sheria hii ambacho kitamlinda mtoa taarifa dhidi ya Kiongozi aliyelalamikiwa ili wananchi waweze kutoa taarifa muhimu kwa urahisi na kuweza kuisaidia Tume kuwapata Viongozi ambao wanavunja misingi ya maadili ya uongozi.

4. Katika sheria hii, hakuna utaratibu maalumu uliowekwa wa kuchunguza mali za viongozi kwa undani. Imeonekana Tume ya Maadili inachunguza pale itakapoona inahitajika au iwapo Tume hii itakuwa na shaka tu bila kuwa na utaratibu maalumu wa kufuata. Hii inatokana na wingi wa viongozi na idadi ya wafanyakazi wa Tume hii wanaoweza kukagua mali na madeni ya viongozi.

   Kwa mnasaba huo, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza kuwepo kwa kifungu ambacho kitaweka utaratibu maalumu ambao utaweka muda maalumu ndani ya Sheria hii, wa kuchunguza mali za viongozi kwa kufanyiwa ukaguzi mali hizo pamoja na matumizi ya viongozi hao. Kwa mfano, kila baada ya mwaka mmoja, mali za Viongozi Wakuu kama vile Rais, Mawaziri, Naibu Mawaziri, nk. zitafanyiwa ukaguzi wa kina. Na kila baada ya miaka miwili, mali za Viongozi wa Taasisi zote zitafanyiwa ukaguzi maalumu na utaratibu huu utaendelea kwa ngazi zote za uongozi. Utaratibu huu unaweza kusaidia Tume kuweza kusimamia maadili ya viongozi vizuri.

5. Katika kusimamia maadili ya Viongozi ndani ya taasisi za umma, imebainika kuwa hakuna mfumo au taratibu maalumu unaotumika katika kusimamia maadili ya viongozi ndani ya taasisi hizo. Hivyo, inapendekezwa kuwepo kwa utaratibu maalumu ndani ya Sheria hii ambao utatoa nguvu kwa Tume ya Maadili kuhakikisha kuwa kila Taasisi ya Umma inaanzisha utaratibu wa kusimamia maadili ya Viongozi katika taasisi hizo pamoja na kuimarisha mfumo wa kupokea malalamiko kutoka ndani ya Taasisi hizo za Umma, badala ya kusubiri malalamiko kutoka kwa wananchi moja kwa moja.

6. Katika sheria hii, kifungu cha 41 kinaeleza kuwa mabadiliko yoyote yanayohitajika kufanyiwa Sheria hii, lazima mabadiliko hayo yafikishwe Baraza la Wawakilishi na yapitishwe na Baraza ndipo yaweze kufanya kazi. Utaratibu huu umeonekana kuwa unachelewesha Tume kufanya mbadiliko hata madogo madogo, jambo ambalo linapelekea kuzorotesha utendaji wa kazi zake. Hivyo, inapendekezwa kuwa na utaratibu ambao utaharakisha kusikilizwa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria hii kwa kuweka utaratibu maalumu wa kusikilizwa mapendekezo na marekebisho madogo madogo yanayohitajika kufayiwa katika Jadweli za Sheria hii. Inapendekezwa kuwa Mheshimiwa Waziri husika kupewa uwezo wa kisheria wa kufanya marekebisho madogo madogo katika Jadweli kwa kushirikiana na Tume ya Maadili ya Viongozi, na baada ya hapo mabadiliko hayo yawasilishwe kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kupata idhini kabla ya kuanza kutumika.

7. Baada ya kufuatia marekebisho ya kifungu cha 41 cha Sheria hii, Tume inapendekeza pia Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kwa kutumia

utaratibu huo huo uliowekwa katika kifungu cha 41 iweze kuwa na mamlaka ya kuongeza masuala mengine ambayo watayaona yanafaa kuongezwa katika fomu za kutaja mali na madeni kwa viongozi.

8. Wahusika wa kutangaza mali pamoja na madeni waliotajwa katika Sheria hii ni Viongozi mwenyewe pamoja na wenza wao na watoto walio chini ya miaka 18. Utaratibu huu umeonekana kutoa mwanya kwa viongozi kuficha mali zao kwa watoto wao walio juu ya miaka 18. Hivyo, Tume inapendekeza kuwa ndani ya Sheria hii, kuwepo kwa kifungu ambacho kitaweka utaratibu wa kuchunguzwa mali za watoto wa Viongozi bila ya kuangalia umri wao, jambo ambalo litasaidia kufichua mali za viongozi ikiwa zitakuwa zikifichwa kupitia watoto wao wenye umri wa Zaidi ya miaka kumi na nane.

9. Katika Sheria hii hakuna kifungu maalumu ambacho kinaelezea kwa kina juu ya kosa la mwenza au mtoto wa kiongozi kusababisha kiongozi kuvunja sheria hii kwa kushindwa kujaza fomu ya kutangaza mali na madeni. Hivyo, Tume inapendekeza kuwekwa kwa kifungu maalumu ambacho kitaelezea kuwa iwapo mwenza au mtoto atasababisha Kiongozi wa Umma kushindwa au kuchelewesha kujaza fomu za kutaja mali na madeni, basi hilo liwe ni kosa ndani ya Sheria hii.

10. Katika Sheria iliopo hivi sasa, kumekosekana kwa baadhi ya tafsiri ya maneno ambayo ni muhimu katika kueleza maana halisi iliyokusudiwa ndani ya Sheria. Hivyo Tume inapendekeza maneno yaliyokuwa hayapo wazi na hayakuwekewa tafsiri basi yatafsiriwe katika kifungu cha pili cha Sheria. Maneno hayo ni kama vile ‘’ulevi wa kupindukia’’, ‘’uhakiki’’ na ‘’uchunguzi’’ na mengineyo.

**11.** Uzoefu wa nchi mbali mbali umeonesha kuwa watendaji wanaohusika na kupokea fomu za tamko la mali na madeni nao husimamiwa katika kutangaza mali zao pamoja na kukaguliwa. Kwa upande wa Zanzibar hakuna chombo hicho ila Sheria inaelekeza Rais kuweka utaratibu wa kutangaza mali za Mwenyekiti na Makamishna wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Hivyo, Tume ya Kurekebisha Sheria inapendekeza kuwepo na chombo maalumu (kama vile Kamati Maalumu kutoka Baraza la Wawakilishi au Bodi maalumu itakayoundwa kwa ajili ya kusimamia kazi hiyo) ambacho kitapokea fomu za kutangaza mali na madeni na kitawakagua watendaji wa ndani wa Tume ya Maadili ya Viongozi ambao wanahusika na ujazaji wa fomu za mali na madeni.

12. Imebainika kuwa utekelezaji wa Sheria hii umekua mdogo kutokana na kukosekana kwa kanuni za Sheria hii. Hivyo Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza Kanuni muhimu katika kutekeleza Sheria hii zitungwe kwa haraka ikiwemo kanuni za kuondosha mgongano wa kimaslahi na kanuni za upokeaji wa zawadi kwa Viongozi.

13. Tume ya Kurekebisha Sheria inapendekeza kuwekwa kwa kifungu mahsusi ndani ya Sheria hii kitakachoelekeza kwa mamlaka husika za uteuzi, kabla ya kufanya uteuzi kuzingatia sifa maalum za kuteua wateule hao. Baadhi ya sifa hizo zinaweza kujumuisha zifuatazo :

a) Awe mzalendo
b) Asidharau nchi yake na kuwadharau Wazanzibari wenyewe.
c) Mwenye mawazo ya maendeleo na kujenga nchi.
d) Awe muadilifu.

e) Awe mtu mwenye maadili na kufuata tamaduni za nchi.

f) Awe mtu mwenye bidii na uwezo wa kufanya kazi (compentency).

g) Awe hajawahi kutiwa hatiani kwa kosa la udhalilishaji, kosa linalohusiana na kodi, kosa la dawa za kulevya na kosa linalohusiana na uaminifu.

h) Awe hajawahi kuhukumiwa kifungo kuanzia miezi sita au zaidi.

i) Awe hajawahi kuhukumiwa kwa makosa yoyote ya jinai na madai.

14. Tume ya Kurekebisha Sheria inapendekeza Sheria hii iongezwe vifungu mbali mbali vikiwemo:

a) kifungu ambacho kitaeleza wazi wazi kuwa Kiongozi wa Umma anatakiwa kufuata Sheria zote za nchi.

b) kifungu ambacho kitawataka Viongozi wote wa Umma kufuata misingi mikuu ya Maadili ya Utumishi wa Umma ambayo imeelezewa katika kifungu cha 4 cha Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya 2011 nayo ni:

i) kujielekeza katika malengo ya kazi;

ii) kujielekeza kwa mpewa huduma;

iii) kujielekeza katika kushiriki;

iv) kujielekeza katika thamani ya fedha;

v) ugawaji wa madaraka;

vi) wajibu wa kuitumikia mamlaka ya Nchi.

c) Kifungu ambacho kitawataka Viongozi wa Umma kufuata miiko katika majukumu ya kazi husika pamoja na kufuata miiko ambayo imeorodheshwa katika kifungu cha 5 cha Sheria ya

Utumishi wa Umma Namba 2 ya 2011. Miiko hiyo ni kama ifuatayo:

i) maamuzi ya uajiri katika utumishi wa umma wa Zanzibar yatafanywa bila ya kujuana, upendeleo au utashi wa kisiasa;
ii) uteuzi na upandishwaji vyeo katika afisi za utumishi wa umma wa Zanzibar utafanywa kwa misingi ya kuwa na sifa;
iii) muundo wa utumishi wa umma wa Zanzibar utazingatia kwa kadri itavyowezekana mchanganyiko wa watu wa Zanzibar;
iv) utumishi wenye ufanisi na uwajibikaji;
v) utoaji bora wa huduma;
vi) utiifu kwa serikali unaendelezwa;
vii) bidii ya kazi inazingatiwa;
viii) nidhamu na kanuni za maadili na uadilifu wa hali ya juu;
ix) heshima kwa wote inafuatwa na kwa usahihi;
x) kuheshimu sheria;
xi) matumizi sahihi ya taarifa rasmi;
xii) uimarishaji na uendelezaji wa kiwango cha juu cha maadili ya kitaaluma;
xiii) uimarishaji wa matumizi bora na sahihi ya rasilimali;
xiv) utoaji wa huduma lazima uwe sawa, huru, haki na bila ya upendeleo;
xv) mahitaji ya watu ni lazima yatimizwe na watu washajiishwe kushiriki katika utungaji wa kisera;
xvi) utumishi wa umma lazima ukidhi misingi ya uwajibikaji;
xvii) uwazi lazima upatikane kwa kuwapa wananchi taarifa zinazopatikana kwa wakati, urahisi na uhakika;

xviii) usimamizi mzuri wa rasilimali watu na kukuza ujuzi, kwa kutumia ujuzi wa juu wa watu waliopo.

d) Kiwekwe kifungu maalumu ambacho kitamtaka kila Kiongozi wa Umma kuzingatia muongozo wa kanuni za maadili ya utumishi wa umma na kanuni za maadili ya kitaalamu au fani zilizowekwa maalumu kwa ajili ya taaluma au fani fulani kama kifungu cha 7 cha Sheria Nam 2 ya 2011 kinavyoeleza. Kifungu hiki kinamtaka muajiriwa yeyote wa umma lazima afuate kanuni za maadili ya utumishi wa umma hivyo kifungu hiki kiwepo kwa kila Kiongozi wa Umma. Kama ilivyo kwa mtumishi wa umma, basi kifungu kieleze hivyo hivyo kwa kila Kiongozi wa Umma kwamba lazima :

i) awe mwaminifu na mwenye uadilifu;

ii) afanye kazi kwa tahadhari na bidii;

iii) katika utekelezaji wa ajira ya Utumishi wa Umma ampe kila mtu heshima na nidhamu na asibughudhiwe;

iv) atekeleze maelekezo halali na yanayokubalika yaliyotolewa na mtu aliyeidhinishwa na Wakala wa muajiriwa ambaye ana mamlaka ya kutoa maelekezo hayo;

v) atunze usiri unaotakiwa wakati wa kufanya mahusiano rasmi ambayo muajiriwa atafanya na waziri au mfanyakazi yeyote wa Wizara;

vi) aweke wazi na achukue hatua muafaka za kuepusha mgongano na muajiri wake katika utumishi wa umma;

vii) asitoe taarifa za uongo au za kupotosha wakati anapotakiwa kutoa taarifa rasmi zinazohusiana na uajiri

katika utumishi wa umma; Uhusiano na utumishi wa kisiasa. Kanuni za maadili ya Utumishi wa Umma.

viii) asiwe na matumizi mabaya ya:

(i) taarifa za ndani;

(ii) kazi za muajiriwa, hadhi, uwezo au mamlaka kwa ajili ya kujipatia au kutafuta kujipatia faida au manufaa kwa muajiriwa au mtu mwengine yeyote;

(iii) afisi yake kufanya udhalilishaji wa kijinsia dhidi ya muajiriwa mwenzake, awe wa ngazi ya juu au ngazi ya chini au dhidi ya mtu mwengine yeyote anayetafuta ajira au huduma zinazotolewa na afisi ya utumishi wa umma;

ix) kwa wakati wote ajiweke katika njia ambayo atadumisha maadili mema ya utumishi wa umma, uaminifu na heshima nzuri ya utumishi wa umma;

x) afuate masharti ya tabia nyengine yoyote iliyoelezwa katika kanuni.

e) Kiwepo kifungu ambacho kitaweka wazi makosa na hatua za adhabu iwapo Kiongozi atachelewesha kujaza tamko la mali na madeni, iwapo atajaza taarifa za uongo au iwapo atashindwa kabisa kujaza tamko la mali na madeni. Hivyo, hatua za adhabu zitakazochukuliwa ziwe wazi.

f) Kiwepo kifungu ambacho kitaeleza kuwa iwapo Kiongozi ametakiwa kujaza tena tamko la mali na madeni (baada ya tamko la mwanzo kuwa halijakamilika au lilikua na taarifa za uongo) na Kiongozi huyo akawasilisha tena kwa mara nyengine tamko likiwa halijakamilika au kuweka tena taarifa za uongo, Tume ya

Maadili ya Viongozi wa Umma waitake mamlaka yenye dhamana ya kiongozi huyo kumsimamisha kazi (*suspension*) kwa kipindi cha mwezi mmoja bila ya malipo na kutakiwa kujaza tena tamko hilo ndani ya kipindi cha siku saba.

g) Kuwepo kifungu ambacho kitamtaka kila Kiongozi wa Umma kufikia malengo yaliyowekwa na Serikali katika taasisi yake pamoja na kuwa mbunifu katika utekelezaji wa kazi zake.

15. Imebainika kuwa jamii inakosa muamko kwa kushindwa kuona utekelezaji wa Sheria hii kwani adhabu wanazopewa viongozi huwa hazitangazwi katika jamii. Hivyo, inapendekezwa Tume kuandaa utaratibu ambao utatoa taarifa za Viongozi ambao wamevunja maadili na kuweza kupewa adhabu ili iwe fundisho kwa viongozi wengine na utekelezaji huu utaweza kutoa muamko kwa jamii.

## 1.2 MAPENDEKEZO YA KIUTENDAJI:

1. Imebainika kuwa Tume ya Maadili haina wachunguzi wenye sifa na utaalam wa fani mbali mbali zinazohitajika katika kufanya kazi zao wakiwemo wathamini wa mali zinazotangazwa na viongozi. Hivyo, inapendekezwa kuwa Tume iwezeshwe kuwa na wachunguzi wenye sifa mbali mbali ili waweze kufichua mali na vitendo wanavyofanya baadhi ya viongozi wa umma ambao si waaminifu. Aidha, uchunguzi ufanyike kwa maeneo maalumu na wachunguzi wawe na taaluma tafauti kwa kila kada za kiuchunguzi.

2. Vile vile, idadi ya wafanyakazi waliopo ni kidogo kulinganisha na idadi ya viongozi waliopo hivi sasa hivyo, inapendekezwa idadi ya wafanyakazi kuongezwa ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi.

3. Kwa kuwa ili Tume ya Maadili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi lazima Tume hiyo iwe na mashirikiano ya karibu na taasisi nyengine za Serikali ambazo zinasimamia maadili ya watendaji kama vile Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA). Hivyo, inapendekezwa kwa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma kujiwekea utaratibu mzuri wa kushirikiana na taasisi hizo nyengine za Serikali ambazo zinaingiliana katika utendaji wa kazi zao ili waweze kurahisisha utendaji wa kazi hizo.

4. Vile vile, katika suala la kutoa elimu kwa umma, inapendekezwa kuwa Tume ya Maadili ishirikiane na Taasisi nyengine zikiwemo Asasi za Kiraia katika kutoa elimu kuanzia ngazi za chini kupitia Maskulini mpaka kwa wafanyakazi wa Serikali na Taasisi binafsi.

5. Tume ya kurekebisha Sheria Zanzibar inapendekeza kuwa Tume ya Maadili ya Viongozi wa umma iweke utaratibu wa kujaza tamko la mali na madeni kwa Viongozi wa Umma kwa kutumia njia ya mtandao. Hili litarahisisha na kutoa wepesi kwa Viongozi katika kujaza tamko hilo na itasaidia Tume ya Maadili kuwa na Takwimu za uhalisia ya idadi ya Viongozi ambao wamejaza tamko hilo.

6. Mbali ya Tume ya maadili kusimamia maadili kwa njia ya kutangaza mali na madeni au kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi, inapendekezwa kuwa

Tume ya Maadili ipanue wigo wake na kusimamia maadili kwa ujumla wake, kama yalivyoainishwa katika Sheria.

**6.3 HITIMISHO:**

Kwa ujumla, Zanzibar imepiga hatua kubwa katika kuimarisha maadili ya viongozi wa umma kwa kuanzisha Tume ya Maadili ya Viongozi kwa ajili ya kusimamia maadili ya viongozi wa Zanzibar. Kwa muda mdogo tangu kuianzishwa kwa Tume hiyo, imeweza kufanya mabadiliko mbali mbali yakiwemo ya muundo wa Tume hiyo ili iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi.

Suala la Jamii kuwa na Viongozi ambao wanafuata maadili ni jambo muhimu sana katika kuleta maendeleo na kuinua uchumi wa nchi. Viongozi wanapokuwa na maadili huondosha ubadirifu wa fedha, uhujumu wa uchumi pamoja na kuondoa vitendo vya rushwa ambavyo ni vyanzo vya uchumi kushuka katika Taifa linaloendelea. Hivyo, ni wajibu wa jamii nzima kusimamia maadili ya Viongozi wetu kwa manufaa ya Taifa letu.

Aidha, ili jamii iweze kusimamia maadili ya Viongozi kwa mafanikio, ni lazima wanajamii wapatiwe elimu na kuwa na uelewa wa kutosha juu ya maana ya maadili na vitendo ambavyo hupelekea uvunjifu wa maadili kwa Viongozi. Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ina jukumu kubwa la kuwaelimisha Viongozi wa Umma na jamii kwa ujumla pamoja na kusimamia maadii kwa Viongozi nchini.

Ili Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma iweze kufikia malengo hayo, ni lazima marekebisho ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma yafanyike hasa kwa kubadilisha Muundo wa Tume uliopo hivi sasa kwa kuweka Muundo mpya ambao utatoa nguvu kwa Tume hiyo kufanya kazi zake kama ilivyopendekezwa katika ripoti hii.